

# Hebu tuzungumze kuhusu matatizo yako

Shule zetu zimedhamiria kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote katika mazingira ya kujifunzia ambayo ni salama, jumuishi na yanayojali. Tunathamini kufanya kazi na wazazi na walezi kama washirika wa elimu ya watoto wao.

Mawasiliano kati yako na shule yako ni sehemu muhimu katika elimu ya mtoto wako. Unapaswa kuwa na uhakika kwamba tutakusikiliza na kuyashughulikia matatizo yako, na kushirikiana na wewe ili kutatua malalamiko.

Wasiliana na shule yako haraka kadiri unavyokuwa na matatizo. Kuzungumza na mwalmu wa mtoto wako, mratibu wa darasa, uongozi wa shule au mkuu wa shule ni mahali pazuri kuanza. Wasiliana na shule ili kuweka miadi au ukipenda, tuma barua pepe, piga simu au andika barua.

Unaweza kuombwa kuwasilisha malalamiko yako kwa maandishi ikiwa unahitaji kutuambia masuala mengi au magamu.

## Zungumza na mkuu wa shule yako ikiwa:

- hukuweza kufikia matokeo ya kuridhisha na mwalmu au mfanyakazi
- jambo hilo linahusu mwenendo wa mwalmu au mfanyakazi
- jambo hilo linahusu kitu ambacho kinaathari elimu ya mtoto wako.

## Zungumza na ofisi ya elimu ya mkoa ya shule yako ikiwa:

- unaamini kwamba tatizo lako halijatatuliwa na shule
- jambo hilo linahusu mwenendo wa mkuu wa shule.

Unaweza kupata orodha ya ofisi za mkoa za elimu kwenye tovuti yetu – [education.wa.edu.au/contact](http://education.wa.edu.au/contact)

## Toa malalamiko bila kutaja jina

Unaweza kutoa malalamiko bila kutaja jina, hata hivyo, inaweza kuwa vigumu kulitatua tatizo hilo kama hatuwezi kuzungumza na wewe kwa kina kuhusu malalamiko yako.

## Pata msaada

Kutoa malalamiko kunaweza kuwa vigumu sana kwa baadhi ya watu. Unaweza kupata msaada kwa kupiga simu ya ushauri wa malalamiko kwenye 1800 655 985. Ofisi ya Uhusiano wa Wazazi inaweza kukupatia msaada kwa kuwa kiungo kati ya shule, ofisi ya mkoa ya elimu, huduma kuu, wazazi na walezi, na wadau wa jumuiya ya shule. Unaweza kuwasiliana na Ofisi ya Uhusiano wa Wazazi ili kupata ushauri muda wowote wakati wa mchakato wa kushughulikia malalamiko kwa barua pepe: [parentliaison@education.wa.edu.au](mailto:parentliaison@education.wa.edu.au)

## Jinsi ya kutoa malalamiko au kupata taarifa zaidi:



Wasiliana na shule yako au ofisi ya elimu ya mkoa. Tafuta maelezo ya mawasiliano: [education.wa.edu.au/schoolsonline](http://education.wa.edu.au/schoolsonline)



Piga simu ya ushauri wa malalamiko: [1800 655 985](tel:1800655985)  
saa 2:30 asubuhi (8:30am) hadi saa 10:30 jioni (4:30pm) Jumatatu hadi Ijumaa



Toa malalamiko na fahamu mchakato wa malalamiko: [education.wa.edu.au/complaints](http://education.wa.edu.au/complaints)

Ikiwa hujaridhishwa na namna malalamiko yako yanavyoshughulikiwa au unaamini matokeo hayo hayana msingi, basi unaweza kuomba mapitio huru katika hatua yoyote wakati wote wa mchakato kwa kuwasiliana na Ombudsman Western Australia - [ombudsman.wa.gov.au](http://ombudsman.wa.gov.au)

**Ikiwa una matatizo, kuzungumza na mwalmu wa mtoto wako au mkuu wa shule ni mahali pazuri kuanza.**